

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA**

**19 MEI, 2023**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**KIKAO CHA ISHIRINI NA TISA – TAREHE 19 MEI, 2023**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

## **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **371. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Shule ya Bweni ya Wasichana katika Halmashauri ya Mji wa Kondo.

#### **372. MHESHIMIWA GODWIN EMMANUEL KUNAMBI (MLIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini ujenzi wa majengo yaliyobaki ya Kituo cha Afya Mlimba utakamilika.

**373. MHESHIMIWA DKT. CHARLES STEPHEN KIMEI (VUNJO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga na kukarabati Vituo vya Afya ili kuendana na utekelezaji wa Bima ya Afya kwa wote.

**374. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kuhakikisha Bajeti ya TARURA inazingatia mitandao ya Barabara katika Halmashauri.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**375. MHESHIMIWA DENNIS LAZARO LONDO (MIKUMI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Watumishi wangapi wamefikishwa Mahakamani kwa rushwa, wangapi wameshinda kesi na kurudi kazini 2010 - 2020.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**376. MHESHIMIWA BONNAH LADISLAUS KAMOLI (SEGEREA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, kuna mpango gani wa kutoa elimu ya utunzaji mazingira kwa Wananchi wanaofanya kilimo katika vyanzo na njia za Mito.

**WIZARA YA KILIMO:**

**377. MHESHIMIWA AHMED ALLY SALUM (SOLWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini ujenzi wa Skimu ya umwagiliaji Kata ya Ishololo Wilayani Shinyanga utakamilika.

**378. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta mbegu mpya za Migomba yenye tija na ya kibiashara.

#### **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

##### **379. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia Wavuvi wa Ziwa Tanganyika zana za uvuvi za kisasa.

#### **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

##### **380. MHESHIMIWA MOHAMED ABDULRAHMAN MWINYI (CHAMBANI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Ofisi ya NIDA katika Wilaya ya Mkoani.

#### **WIZARA YA AFYA:**

##### **381. MHESHIMIWA ASIA ABDUKARIMU HALAMGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, hadi sasa hali ya Ugonjwa wa Figo ipoje nchini.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

**382. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Wamachinga wangapi wamefuzu kuwa Wafanyabiashara rasmi kwa kipindi cha kuanzia 2016 hadi 2021.

**WIZARA YA MAJI:**

**383. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, maeneo mangapi yameshabainishwa kuwa ni vyanzo vya maji salama ardhini na hatua gani zinachukuliwa kulinda maeneo hayo.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**384. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani wa kuvuna fisi wanaovamia makazi ya Wananchi, kujeruhi na kuuu Watu katika Kata ya Endamarariek.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**385. MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE  
WAITARA (TARIME VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha VETA Nyamongo Wilayani Tarime.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA  
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA  
19 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**